

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA

11 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA – TAREHE 11 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA
JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

224. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Ibungu – Kafwafwa hadi Kyimo itafanyiwa upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi kwa kuwa imetajwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

225. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

- (a) Je, ni matukio mangapi ya moto yametokea kwenye Shule na Masoko katika kipindi cha miaka mitano iliyopita;
- (b) Je, Uchunguzi uliofanyika ulibaini vyanzo vya moto huo ni nini.

WIZARA YA KILIMO:

**226. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO
MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-
Zao la Kahawa limekuwa likilimwa kwa wingi
katika Jimbo la Hai lakini Zao hilo kwa sasa
limekosa tija:-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati sahihi
kufufua Zao hilo katika Jimbo la Hai.

WIZARA YA MAJI:

**227. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA
KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi
wa Maji wa Katerela kwa ajili ya Kata za
Kasharunga na Rulanda.

**228. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE
(MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya
kuwasaidia Wananchi wa Mji wa Itigi kuweza

kuvuna maji katika Mbuga inayozunguka Mji huo.

229. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kiburubutu katika Jimbo la Kilombero.

WIZARA YA NISHATI:

230. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itaunganisha mfumo wa gesi asilia kwa ajili ya kupata nishati ya kukaangia Samaki katika Soko la Feri Manispaa ya Mtwara Mikindani.

231. MHESHIMIWA DKT. STEVEN LEMOMO KIRUSWA (LONGIDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-
Umeme wa msongo mkubwa wa KV 400 toka Singida hadi Namanga umepita katika baadhi ya maeneo ya wazi na malisho ya mifugo

kwenye Vijiji vya Engikaret, Ranchi, Orbomba, Kimokouwa na Eorendeke; na fedha za fidia ilipendekezwa zitolewe kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Vijiji husika pamoja na watu binafsi ambao umeme huo umepita kwenye makazi yao:-

Je, ni lini fedha hizo zitatolewa.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

232. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Katavi kwani ujenzi huo unakwenda kwa kusuasua.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

233. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro wa Wananchi wa Bugeli na Hifadhi ya Manyara pamoja na mauaji ya Wananchi yanayotokea mara kwa mara.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA
11 MEI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**